

**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA RUKWA MHE.
ZELOTE STEPHEN ZELOTE ALIYOITOA WAKATI WA
MKUTANO NA WAFANYABIASHARA WA MJINI
SUMBAWANGA KATIKA UKUMBI WA LIBORI CENTRE
SUMBAWANGA TAREHE 23 JUNI, 2016**

Mwenyekiti wa TCCIA - Mkoa wa Rukwa,
Katibu Tawala Mkoa,
Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga,
Ndugu Wafanyabiashara na Wakulima,
Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Sumbawanga,
Mkurugenzi wa Manispaa ya Sumbawanga
Viongozi wa Taasisi za Serikali,
Watendaji wa Serikali,
Ndugu Waandishi wa Habari
Wageni waalikwa
Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu
mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha kukutana mahali
hapa.

Aidha, kupitia hadhara hii napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuniteteua kuwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa.

Ninaomba tuzidi kushirikiana kwa Maendeleo ya Mkoa wetu.

Ni takribani miezi sita sasa tangu kikao kilichopita cha wafanyabiashara kilipoketi tarehe 03 Januari, 2016 na kuhudhuriwa na Mkuu wa Mkoa aliyenitangulia Mhe. Magalula Said Magalula.

Jambo ambalo nataka kulisisitiza ni masuala gani ambayo yalikuwa maazimio katika Kikao hicho ambayo kwa sasa tupate utekelezaji wake. Ni maagizo gani kama Serikali tunawataka Sekta binafsi mshirikiane na Serikali ili kukuza Uchumi na kuongeza kipato. Pia ni masuala gani sisi kama Serikali ambayo Sekta binafsi mnapendekeza au kuomba ufafanuzi.

Jambo jingine ni vema tukatambua majukumu na wajibu wa TCCIA, nini mmefanya hadi sasa matarajio yenu kwa baadaye ni nini mnategemea kufanya na mikakati yake.

Matarajio ya Serikali kwa TCCIA ni kuona:-

- Inahudumia Jamii ya Wafanyabiashara na kuwasaidia kuyafikia masoko
- Kuongeza wigo wa Ajira na mazingira ya biashara yenye faida
- Kutengeneza nafasi za ajira na kuwa kichocheo cha ukuaji wa kiuchumi, kupitia Sekta ya biashara, Viwanda na kilimo
- Kwa kifupi TCCIA nimuhamasishaji na muwezesaji wa ukuaji wa biashara.

Serikali inazidi kutoa fursa kwa Sekta binafsi kuweza kutekeleza majukumu yake kwa dhana ya (Public Private Partnership), Serikali ina wajibu wa kuweka mazingira wezeshi kwa Sekta binafsi kuwekeza na kutengeneza faida kwa kufuata miongozo, sheria, kanuni na taratibu.

Ni wajibu wa Serikali kuweka mazingira wezeshi kwa kuwa Sekta binafsi ni mdau muhimu katika Maendeleo kwa kuwa idadi kubwa ya Ajira zipo Sekta binafsi, pia Sekta

binafsi ni walipa kodi wazuri na kuwezesha Serikali kutoa huduma kupitia makusanyo ya kodi.

Hivyo natoa wito kwa Taasisi zote za Serikali pamoja na Wafanyabiashara, kwanza tuone uwezekano wa kufanya kazi pamoja kwa mtazamo chanya, tutambue fursa zilizopo na kuona namna bora ya kuzitumia kwa nguvu ya pamoja.

Katika risala ya Mwenyekiti wa TCCIA kuna baadhi ya hoja zimeibuka ambazo nitaomba, tupate ufafanuzi kutoka Taasisi za Serikali zilizopo mahali hapa.

Asanteni kwa kunisikiliza.

Zelote Stephen Zelote

MKUU WA MKOA

RUKWA